MUNGU ALIYE MWINGI WA REHEMA

Mnaweza kuketi. Nimefurahiwa sana kuja hapa na kumwona Ndugu Moore na wengine wote hapa penye jukwaa; marafiki ambao nimewajua kwa miaka mingi. Hakika ni heshima kubwa kuwaona hapa usiku huu. Najisikia mtu duni kusimama hapa na kuhubiri huku kukiwepo wanatheolojia wakuu nyuma yangu, na huenda wakanisahihisha nikikosea. Natumaini hivyo.

2 Tuna furaha sana usiku huu kuwa na mtu fulani hapa, dada Rose. Tulikuwa tukishuka . . . Nilikuwa pamoja na ndugu Shores na makamu wake, leo, kwa chakula kidogo cha mchana. Na tulipokuwa tukija ndugu William alisema kwamba dada Rose alikuwa mgonjwa sana. Na tukaingia kule kumwona kwa dakika moja tu, tukapiga magoti. Naye alikuwa na homa kali sana, na hawezi kabisa. Maombi madogo tu, na Bwana akanena nasi, na kusema, "Atakuwa mzima, naye atakuwa huko kesho usiku." Naye yupo hapa usiku huu, akiketi papa hapa. Naam.

3 Dada Rose, simama kwa dakika moja tu, ili wao . . . Tunamshukuru Bwana. Alikuwa hawezi kitandani. Akasema, "Shetani ameniweza kwa kila jambo. Nilikuja huku na kuugulia huku", aina fulani ya ugonjwa wa koo na mengineyo. Bali Bwana ameniponya, kwa hiyo tuna furaha. Tukimshukuru Bwana mpendwa!

4 Naam, tumekuwa na nyakati za ajabu. Na kesho usiku, sasa tutaenda kule—kule Ramada. Na msisahau sasa, haitakuwa hapa kesho usiku, itakuwa Ramada. Nao mkutano utaanza usiku ufuatao. Iliwabidi kunistahimili mimi usiku mwingine mmoja, mnajua.

5 Kwa hivyo usiku wa jana nili—nilipita kipimo sana, nami nikajiahidia kidogo ya kwamba tangu mwanzoni mwa mwaka kwamba nitazifupisha jumbe hizi kutoka masaa matatu ama manne, masaa matano, hata labda dakika thelathini ama arobaini. Na kama nilivyowaambia jana usiku, mke wangu alinipongeza Jumapili na kusema, "Ulifanya vizuri sana." Kwa—kwa hiyo basi, hakika ikanibidi kuja huku jana usiku na nikaharibu, mnaona, kuhusu muda. Nilikuja chukua dakika hamsini na tano, badala ya thelathini, usiku uliopita.

6 Tulipokuwa tukishuka kuja huku usiku huu, Billy alisema, "Utahubiri juu ya nini?"

7 Nikasema, "Naam, nina maandishi kidogo yaliyoandikwa hapa, na Maandiko machache. Sijui, baadhi ya mengine, jumbe

nne au tano tofauti." Nikasema, "Najisikia nifikapo chini kule, na kuona yanayoendelea."

8 Akasema, "Uliahidi kuwaombea wagonjwa wao wote." Nikasema, "Naam bwana. Una kadi ngapi?" Akasema, "Mia mbili."

Nikasema, "Yanipasa kuanza nazo usiku huu."

9 Naye akasema, "Sasa kumbuka, utapata tu dakika kumi na tano kuhubiri." Kasema, "Ulichukua zilizobakia jana usiku." [Ndugu Branham na makutano wacheka—Mh.] "Dakika kumi na tano." Itatupasa kuharakisha sivyo?

10 Naam, tuliwaahidi ninyi, ya kwamba tungewaombea wale watu waliokuwa na kadi za maombi, na tuna—tuna wajibu wa kutimiza ahadi, hakika. Hatuwezi kuwapisha wote kwenye mistari hii, wala siwezi kuwaita binafsi, kutoka kwenye makutano. Hata ingawa Roho Mtakatifu angenionyesha, sitaweza kufanya hivyo. Najisikia uzito ndani yangu. Na, lakini sote tumeyazoea mambo hayo. Tunajua Mungu yungali bado Mungu. Siyo kwamba hayo ndiyo yanayoponya. Hayo tu yanayojenga imani, hata tukaweza kujua kwamba tupo katika uwepo Wake.

11 Na jioni hii tutawaombea wagonjwa wote, kila mmoja aliye na kadi ya maombi ili kuombewa. Na ndipo kesho usiku kule Ramada tutajaribu kutoa nyingine na kuanza kuwaombea kule, kwa maana ningali nina usiku wa kesho. Nami nadhani nina usiku mmoja wa mkutano, huenda tukawa na kifungua kinywa pia. Hayo yatategemea jinsi mambo yatakavyotendeka.

12 Kuna wengine, mmoja wa wahubiri ambaye hakuweza kufika; na hata sasa bado hajafika; sidhani, Ndugu Humburg, au huyo. . . [Ndugu mmoja asema "Amburgy"—Mh.] Amburgy, Amburgy, Kash Amburgy. Kwa hiyo nilitamka vibaya, hilo ni jina la Kijerumani. Nahisi hicho ni Kijerumani. Kwa hiyo huenda inanipasa kwa namna fulani kugugumiza jina, kama tunavyosema, samahani kwa hayo matamshi, kwake.

13 Kwa hiyo tumekuwa na wakati wa ajabu katika Bwana, hata hivyo. Kwenu nyote, iwapo kuna wageni hapa usiku huu, tunafurahi kuwa pamoja nanyi, na tunaamini Bwana atawabariki. Naomba ya kwamba pasiweko mgonjwa yeyote katika jengo hili tunapoondoka usiku huu, kwamba Bwana wetu atashuka katika nguvu zake kuu na atawaponya wote walio wagonjwa na wanaoteseka.

14 Hapa wakati fulani uliopita nilizoea kuhojiana na wote mmoja mmoja, baadhi ya mashauri yalikuwa magumu hata hatukuweza kumaliza. Ndipo watu waliongezeka sana, hata ikawa Bwana alizidi kutubariki, hata tukafikia kuwa na watu mia tatu au mia nne waliokuwa wakingojea kuingia kwa zamu. Kwa hiyo watu wengine waliudhika kwa sababu iliwabidi kusubiri. Labda katika muda huo ingekupasa usubiri labda

mwaka mmoja au miwili ili upate nafasi ya kuingia, unaona, katika nafasi kati ya mkutano mmoja na mwingine ili kuwa na mahojiano ya kibinafsi. Nasi tulikuwa tunaketi tu na kumngojea Bwana hata alipotuambia jambo lenyewe hasa lilikuwa nini.

15 Hapana shaka kuna watu wanaoketi hapa usiku huu ambao wamekwishakuwa kwenye mahojiano hayo ya kibinafsi. Wapo? Hebu tuwaone mkiinua mikono yenu. Katika mahojiano maalum. Naam. Wameketi pale basi, nao wanajua kwamba hiyo ni kweli. Tunangoja tu kuona yale ambayo Bwana angenena, jambo gani hilo...Na ilinipasa kukomesha hayo si muda mrefu uliopita. Nilimwambia Billy hatungekuwa na mahojiano mengine ya faragha.

16 Mwaona, ni—nimepita umri wa miaka ishirini na mitano mara ya pili hivi karibuni, na ninakaribia mara ya tatu. Na kwa hivyo unapokuwa mzee kidogo, naam, huwezi, hu...sijui kwanini huwezi kuendelea kama ulivyokuwa zamani. Hatua zako zinafupika. Na—na hakika ndugu Moore hajui chochote kuhusu hayo bado. Yeye...nafikiri tuko karibu umri mmoja.

17 Bali maji mengi yametiririka mtoni tangu mimi na wewe, na ndugu Brown tulipokuja hapa mara ya kwanza, pamoja na ndugu Outlaw na ndugu Garcia, na ndugu Fuller. Sijui kama ndugu hao wamo humu usiku huu? Ndugu Garcia, Ndugu Fuller, Ndugu Outlaw wamo? Inueni mikono yenu kama mmo. Naam huyo ni ndugu Fuller, naamini, kama sijakosea. Ndugu Outlaw yupo hapa. Ndugu Garcia na—naamini ya kwamba amehama Phoenix. Naamini hiyo ni kweli. Ali—alihama Phoenix na yuko huko California. Naam, bila shaka zilikuwa siku zenye fahari, nami ningali nauamini ujumbe ule ule niliokuwa nao wakati huo, "Yesu Kristo, Yeye yule jana, leo na hata milele. Nahisi hiyo imekuwa kama...vema, Becky alikuwa kitoto. Hiyo ni kama miaka kumi na tisa.

18 Na sasa yeye ni mkubwa, amekua, mnene, mwenye sura mbaya akiketi mahali fulani pale, umri wa miaka kumi na tisa. Upo wapi Becky? Jamani, nitajuta kwa kusema hayo. Nakumbuka nilipokuwa nikimbeba mkononi mwangu. Hakika ningekuwa na kazi kubwa kufanya hivyo usiku huu.

19 Nakumbuka kwenye kanisa la ndugu Garcia usiku mmoja, alikuta mtoto mchanga sana. Nami nikasema tuna mkutano wa kimataifa usiku huu. Nikasema, "Ninawazungumzia Wahispania. Na nikasema, "mke wangu hapa ni Mjerumani, Nikasema ni Mu-Irish." Na nikasema, "Na msichana wangu mdogo ni Mhindi," na huyo alikuwa Becky.

20 Ndipo nilipotokea mlango wa nyuma, kulikuweko mtoto wa Ki-mexico kule, akasema "Ndugu Branham!"

Nikasema, "Naam kipenzi, unataka nini?"

Akasema, "Je hudhani mtoto wako ni mweupe kidogo, hawezi kuwa Mhindi?" Yeye ni rangi ya dhahabu, mwajua.

Nami nikasema, “Ni Mhindi kwa tabia.”

21 Basi tunashukuru kwa kuwa hapa tena usiku huu. Basi kabla hatujakaribia Neno, na tumkaribie Yeye, kwa kuwa Yeye ni Neno. Neno linapodhihirishwa, hivyo ni Yeye ndani Yako.

22 Kama tulivyohubiri jana usiku juu ya *Mbegu Yenye Hitilafu*, mlipendezwa na hayo, baraka za Bwana? [“Amina”] Nili—nilipendezwa kuwaletea ujumbe huo. Na tumeona zile mbegu ni nini.

23 Naam, sasa kuna haja maalum usiku huu, jambo maalum? Labda wengine wenu ambao mtakuwa kwenye msitari huu wa maombi, mseme “Mungu nirehemu. Nijapo kuombewa, na imani yangu iongezeke ipate kutosheleza masharti yale.” Na—na huenda ikawa mtu fulani ana mtu ampendaye, ni mgonjwa ama chochote kile, waweza kuinua mkono wako ili Mungu atazame chini na kusema . . . Sasa kama hivyo . . . Hamjui jinsi inavyonifanya nijisikie kutazama kule. Tazama tu mahitaji humu! Ndugu watumishi, tazameni hayo tu. Mwaona? Sasa, kama inanifanya nijisikie hivyo, inamfanyaje Baba yetu? Hakika.

Na tuombe sasa.

24 Yesu mpendwa, tunakaribia sasa kile kiti kikuu cha Enzi cha rehema, kwa Jina hili linalotosheleza kabisa. “Kwa maana hapana jina jingine walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo, bali hili Jina la Bwana Yesu pekee”. Nasi tunakuja katika Jina Lake. Nasi twaomba, Baba uliye mbinguni utupokee usiku huu kama watoto wako wanaokuamini. Na utusamehe kutokuamini kwetu Bwana. Saidia hilo usiku huu, ili iwe kwamba tutaamini kabisa kila Neno la Mungu usiku huu, kwa mambo yote tunayohitaji.

25 Unajua yote yaliyo chini ya mikono hii iliyoinuliwa; kuna magonjwa, labda wengine wao ni shida za kinyumbani, wengine wao ni shida za kifedha, wengine wao uchovu, labda wengine walianguka, wengine ni wenye dhambi. Hata iwe shida gani. Wewe u zaidi ya adui yeyote. Kwa hiyo tunaomba Bwana, ya kwamba—ya kwamba usiku huu, kwamba tutatambua kuwa maadui zetu, kila mmoja amekwishashindwa, na hata kifo chenyewe. Na kwamba sisi tu zaidi ya washindi katika yeye yule—yule aliyetupenda na akajitoa Nafsi Yake kwa ajili yetu, Naye ametuosha katika Damu yake.

26 Tunaomba, Bwana, kwamba kutokuamini kote, mashaka yote, mapingamizi yote, na yale yote yasiyofanana na Mungu yatukimbie usiku huu, ili Roho Mtakatifu apate mamlaka mioyoni mwetu. Twaomba azungumze nasi katika njia za ajabu. Na aseme nasi katika uweza wake. Na awafufue wale walio—waliokufa rohoni. Awaponye walio wagonjwa na wanaoteseka, ukawainue wenye magoti manyonge, viwete. Na pawe na wakati wa kuburudika.

27 Na ianze usiku huu, Bwana, tuondoke hapa kwenda Hoteli ya Ramada na kuanzisha mmoja kati ya mikutano mikuu sana iliyowahi kuwako katika mji huu. Bwana, tunapokutanika pamoja na kuomba, Ulisema, "Ikiwa watu walioitwa kwa Jina Langu, watajikusanya wenyewe pamoja na kuomba, ndipo Nitasikia kutoka Mbinguni." Na, Mungu, tunaomba usiku huu iwe hivyo.

28 Sasa, Baba, tunaposoma Neno, hapana anayeweza kulifasiri ila wewe. Wewe ndiye unayefasiri Mwenyewe, nasi tunaomba utufasirie mambo tusomayo usiku huu, kwa maana twaomba katika Jina Lake Yesu. Amina.

29 Basi kama wengi wenu wanataka kuandika Maandiko ambayo mhudumu atasoma. Na ningependa ninyi jioni hii, kama mkipenda, mfungue Waefeso.

30 Nami nilikuwa nikihubiri Jumapili iliyopita juu ya Waefeso, ambavyo kitabu cha Joshua ndicho Waefeso ya Agano la Kale, na ambavyo kilikuwa kitabu cha ukombozi.

31 Na ukombozi una sehemu mbili tofauti, "Kutoka kwa" na "Kuingia ndani ya." Kwanza, yakupasa kutoka. Watu wengine wanataka kuingia pamoja na ulimwengu; bali yakupasa kutoka kwenye ulimwengu, kuingia katika Kristo. Inakupasa utoke kwenye kutokuamini, uingie kwenye imani. Hapawezi kuwa kitu chochote njiani mwako. Inakupasa kuacha kabisa nyuma mambo yote yanayopingana-pingana na Neno la Mungu, ili kuingia katika imani.

32 Na hicho kilikuwa kitabu cha Waefeso cha Agano la Kale, Yoshua. Ambapo Musa aliwakilisha sheria, ambayo haingelimwokoa yeyote, bali neema ingeliokoa. Na hapa *Yoshua* ni neno lile lile kama Yesu, "Yehova Mwokozi."

33 Na sasa basi, tunaona kwamba tumekuja katika Waefeso nyingine, Waefeso nyingine sasa. Ambapo basi katika madhehebu yetu ya kiakili na mengineyo, na mipango yetu yote ya elimu, imekuja kwenye Yordani ya—yake, ndipo inatupasa kuwa na—na Waefeso tena. Inatupasa tuwe na kutoka, "Kutoka nje" na "kuingia ndani ya," kwa ajili ya kunyakuliwa.

34 Basi tutasoma jioni hii kutoka sura ya pili ya Waefeso. Nilikuwa nikisema hayo tu ili mfungue ma—mahali hapo, ama mfungue hiyo sura.

> *Ninyi, nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu;*
>
> *Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi,*
>
> *Ambao zamani sisi sote nasi tulienda kati yao katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na*

ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine.

Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda,

Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu, alituhuisha pamoja Naye au *ahituhuisha pamoja na Kristo (mmeokolewa kwa neema.)*

35 Nataka kuchukua kutoka hapo machache ama sehemu ya aya ile, "bali Mungu," *Mungu Aliye Mwingi wa Rehema.*

36 Nataka ninyi mwone hapa ambavyo nabii, mtume, namaanisha Paulo, ambaye—ambaye, alivyotaja hili, ambavyo, "Ninyi amewahuisha mliokuwa wafu. Ninyi amewahuisha ambao hapo kwanza mlikuwa wafu, wafu katika dhambi na makosa; mkifuata mambo ya ulimwengu, mapenzi ya mwili, na mkitimiza mapenzi ya nia. Ame . . . "

37 Ni nini kilichosababisha mabadiliko haya mnaona? Ni nini kilichosababisha hayo, "kutoka wakati mlipokuwa wafu", hata kuhuishwa? *Kuhuishwa* maana yake ni "kufanywa hai." Kulikuwako mabadiliko kutoka mautini kuingia uzimani. Hakuna lingine, hakuna jambo lingine linaloweza kutendeka kwa mtu yeyote, kubwa hivyo, hata kumbadilisha kutoka mautini kuingia uzimani. Mtu, kama alikuwa katika kufa kimwili, yeye angeliponywa mwili, hilo lingekuwa jambo kubwa sana, bali hakuna jambo kubwa kama aliyekuwa mfu kiroho na Mungu akamhuisha akawa hai.

38 "Ninyi mlikuwa wafu wakati uliopita." Mlikuwa wafu. Hata wengi hapa usiku huu, wakati mmoja mnaweza kutazama nyuma na kuona kuwa mlikuwa wafu. Bali sasa mbona ninyi si wafu usiku huu, kama mlivyokuwa wakati huo? Inakupasa kuwa hivyo kwa maana ulikuwa mwenye dhambi, "bali Mungu aliye mwingi wa rehema." Hilo ndilo—hilo ndilo jambo lenyewe. "Mungu aliye tajiri." Mambo haya yote tuliyokuwa, "Lakini Mungu"! Hii ilibadilisha mambo papo hapo; "Mungu Aliye mwingi wa rehema"!

39 Jamani, nafurahia hayo, ya kwamba Yeye ni mwingi wa rehema. Kama angalikuwa mwingi wa pesa, kama angalikuwa mwingi wa mali, na ndivyo alivyo, bali jambo kubwa mno ni kuwa mwingi wa rehema. Jamani, hilo ni neno bora namna gani, ambavyo tulikuwa wafu hapo kwanza.

40 Na kama tulivyohubiri usiku uliopita, ambavyo ile mbegu haina budi kufa. Na chochote karibu na hiyo chembechembe ya uhai, ni lazima, si kufa tu, bali pia kuoza kama kisipooza hakitaweza kuishi. Na *kuoza* ni "kuharibika kabisa; Imekwisha." Na hata tutakapofikia mahali ambapo maoni yetu na mawazo yetu yamekwisha kabisa na kuoza kabisa kutoka ndani yetu, ndipo chembechembe ya uhai itaweza kuanza kuishi.

41 Sasa—sasa huenda sisi, huenda nikaingiza fundisho dogo hapa. Lakini si...kama huamini, vema. Hilo ni sawa tu. Mimi naliamini. Naamini ya kwamba—kwamba binadamu anapozaliwa katika ulimwengu huu, anapokuwa mtoto mchanga, aliyezaliwa ulimwenguni, hungeweza kuwa hapa bila ya Mungu kujua tangu milele, kwa sababu Yeye hana mwisho, Yeye anajua mambo yote. Na huyu mtoto mdogo anapozaliwa ulimwenguni, kuna kitu ndani ya mtoto huyo mchanga. Iwapo atapata uzima, kuna kitu kidogo ndani mle katika mtoto huyo, ambacho lazima atakifikia. Hiyo mbegu ndogo imo ndani yake. Sasa kama mtachukua . . . Maandiko yanaeleza hayo waziwazi.

42 Basi kama una Uzima wa Milele usiku huu, kama una Uzima wa Milele, basi ulikuweko daima, kwa maana kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Tulikuweko daima. Na sababu ya kuweko kwetu, ni kwamba tulikuwa sehemu ya Mungu. Na Mungu ndiye tu kitu kilicho cha Milele.

43 Na kama Melkisedeki alivyotwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimu, na hiyo ikahesabiwa kwa kitukuu wake Lawi, aliyekuwa bado viunoni mwa Ibrahimu; akalipa sehemu ya kumi, alikuwa bado viunoni mwa Ibrahimu wakati alipokutana na Melkisedeki. Nataka kuhubiri hayo kule kwingine, asubuhi moja. *Je huyu Melkisedeki ni Nani?* Tazama hayo. Zamani sana, Mungu alimjua huyu mvulana akishuka kuja. Yeye ajua mambo yote.

44 Sasa, sisi ni sehemu ya Mungu. Wewe umekuweko siku zote. Hukumbuki, kwa sababu ulikuwa wazo tu ndani ya Mungu. Ulikuwa tu mawazoni mwake. Jina lako hasa, kama liliwahi kuwemo katika kitabu cha uzima, liliwekwa pale kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Alijua wewe ulikuwa nini.

45 Ninasema tu hili, si ili kuvuruga mafundisho, bali kuyanyosha, ili tupate kuacha huu woga pamoja na hofu. Hamjui ninyi ni akina nani. Hamwendi kuwa, bali ninyi ni wana wa Mungu sasa. Mwaona, daima ninyi mmekuwa wana wa Mungu. Mnaona?

46 Wakati ulipokuwa ndani ya mawazo ya Mungu hapo mwanzoni, inapaswa uwe, yaani sehemu yako fulani, ule uzima ulioko ndani yako sasa, ulipaswa uwe na Mungu hapo mwanzoni. Basi, wakati Yeye, kabla hata wewe hujafanyika mwili hapa duniani, kabla hapajakuweko chochote isipokuwa Mungu, wewe ulikuwa mojawapo ya mawazo yaliokuweko ndani Yake. Alijua jina lako lingekuwa nani. Alijua rangi ambayo nywele zako zingekuwa nayo. Alijua mambo yote kukuhusu wewe. Jambo lililotendeka ni wakati wewe, ulipokuwa ungali mwenye dhambi . . .

47 Wengi wenu wanaweza kushiriki pamoja nami juu ya wazo hili. Ulipokuwa mvulana mdogo, au msichana mdogo, ungetembea huku na huko, na kungekuwa na mambo fulani

ambayo tu, ambapo hayangaliudhi watoto wengine, ilionekana kama kwamba kulikuweko na kitu ndani yako ambacho kililia. Kulikuwepo Mungu mahali fulani, bali wewe ulikuwa mwenye dhambi. Je unakumbuka hayo? [Makutano wanasema, "Amina"—Mh.] Hakika. Sasa je, hiyo ilikuwa nini? Hiyo ilikuwa ile chembe ya Uzima ndani yako wakati huo.

48 Ndipo baadaye kidogo ukasikia Injili. Labda ulienda kanisani ulichukua *hili* na *hilo,* na kuenda dhehebu moja hadi lingine. Bali siku moja, kwa kuwa ulikuwa sehemu ya Mungu, ilikupasa uwe sehemu ya Neno. Na uliposikia Neno, ulijua ulikotoka, ulijua Ukweli. Ulikuwa hivyo tangu awali, ile mbegu ilikuwa ndani yako tangu awali. Neno liliona Neno lililokuwa ndani yako, lililokuwako kabla ulimwengu kuwekwa misingi, likaona lile Neno na ukaja Kwake.

49 Kama ile hadithi yangu ndogo ya tai aliyeanguliwa na kuku. Naye kifaranga huyo wa tai akatembea na vile vifaranga vya kuku, yeye, kuku, alipolia tai hakuelewa mlio wake. Na—na wale vifaranga, chakula walichokula kwenye kitalu, ha—hakukielewa, jinsi walivyofanya hayo. Bali kulikuweko kitu fulani ndani yake, kilichoonekana kama tofauti na yule kuku alivyokuwa, kwa sababu tangu mwanzo yeye alikuwa tai. Naam. Siku moja mama tai akaja akimtafuta, na, aliposikia huo mlio wa tai, ulikuwa tofauti na ule mlio wa kuku.

50 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kila mwamini aliyezaliwa mara ya pili. Unaweza kusikia theolojia yote unayotaka, na kila hitilafu iliyoanzishwa na mwanadamu, lakini hili Neno lilipoangaza pale, ulikijia kile kitu kilichokuwa kimeshikilia. "Nanyi mliokuwa wafu katika dhambi, Amehuisha huo uzima." Inapasa uwepo uzima kwanza ndipo upate kuhuishwa. Mungu kwa kujua Kwake tangu milele, alijua mambo yote. Nasi tulichaguliwa kuwa wana na binti Zake Mungu. "Ninyi mliokuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu, ambamo tuliishi katika siku zetu zilizopita, bali Yeye ametuhuisha."

51 Mtazame Paulo, Paulo alipokuwa mtheolojia mkuu. Bali alipokutana na lile Neno uso kwa uso, Yesu, alihuishwa. Akawa hai upesi sana, kwa sababu yeye aliamriwa kuwa hivyo. Lile... Yeye alikuwa sehemu ya Neno, na Neno lilipoona Neno, liliona tabia yake. Ule mlio wote wa kuku katika makanisa haya ya kawaida, ulikuwa bure kwake; yeye alikuwa ameona Neno, Neno lilikuwa sehemu yake. Alikuwa tai. Hakuwa kuku, alikuwa tu kwenye kitalu pamoja nao. Bali yeye alikuwa tai tangu mwanzo.

52 Nilisikia hadithi ndogo kama hiyo, natumaini sionekani mwenye kukufuru, habari za kifaranga cha bata kilichoanguliwa na kuku, wakati fulani. Hakikuelewa. Kiumbe kidogo cha kuchekesha, kitu ovyo, hakikuelewa mavumbi na kila kitu. Walikuwa wakicheza kwenye kitalu. Bali siku moja kizee

kuku aliwatoa na kuwaongoza vifaranga vyake nje nyuma ya kile kitalu, ndipo (yule bata mdogo) akasikia harufu ya maji. Akatimua mbio upesi alivyoweza kuyaelekea yale maji. Kwa nini? Yeye hakuwahi kuwa kwenye maji hapo awali. Bali alikuwa bata tangu mwanzo. Jambo tu lililompasa kutenda ni kujitambua.

53 Mwamini ni vile vile. Kuna kitu ndani yake, ambacho, unapokutana na Mungu uso kwa uso, anazingatia moyoni mwake. Mbegu hiyo imo ndani yake, nayo inahuishwa. Jamani, ndivyo naye anavikimbia vitu vya ulimwengu. Vimekufa kwake. Naam, nakumbuka jinsi ambavyo sote katika maisha yetu ya zamani tuliishi katika hivyo vitu vya ulimwengu. Bali tulipopata kile kitu halisi, kitu fulani kikatuhuisha, mbegu ndogo ikawa Hai, ndipo mambo yote ya ulimwengu yakaoza papo hapo. Hatukuvitamani tena.

54 "Yeye aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi. Mwenye kuabudu akiisha kusafishwa mara moja, hatajiona tena kuwa ana dhambi, hana tena tamaa ya kutenda dhambi." Habari za dhambi zimekwisha. Umekuwa sehemu ya Mungu, katika Kristo. Kristo alikufa kukukomboa.

55 Sasa hebu fikiri yote yale tungelikuwa kama si Mungu. Bali Mungu, katika wingi Wake wa rehema, jinsi alivyokwisha kutukomboa usiku huu! Tungelikuwa wapi usiku huu kama si kwa rehema Zake Mungu nyingi kwetu?

56 Wakati mmoja ulimwengu ulikuwa wenye dhambi sana, mwanadamu alikuwa ameuharibu hata Mungu akaghairi kuwa alimuumba mwanadamu. Kichwa chote kilikuwa donda lililooza na kunuka, mwili mzima. Mungu alijutia kumuumba mtu. Ndipo akasema, "Nitamwangamiza huyu mtu Niliyemuumba." Atawaangamiza kwa sababu hawana kitu isipokuwa tu upotovu mtupu.

57 Binadamu wote wangaliangamizwa kabisa wakati huo, bali Mungu, aliye mwingi wa rehema, hangelimwachilia asiye na hatia kuangamia pamoja na mwenye hatia. Ndipo akaondoka akafanya njia iliyoandaliwa kwa wale waliotaka kuingia, waliotaka kutenda haki. Aliandaa njia ya rehema kwa wale waliohitaji rehema, na kuwatayarishia safina. Kwa maneno mengine, Yeye aliwatia tai Wake mabawa, ili wasizame pamoja na kuku. Bali Yeye—Yeye akaweka mlango wa kutokea katika siku za Nuhu. Hii ilimfanya Yeye afanye hivyo, kuwapa mlango, kwa maana Yeye alikuwa mwingi wa rehema.

58 Bali baada ya kuwawekea watu wake mlango nao wakakataa, sasa, sababu ya kukataa kwao ni kwa maana hakikuweko kitu ndani yao cha kuupokea. Hamna kitu cha kuupokea. Mama yangu alizoea kusema, "Huwezi kupata damu katika mboga nyekundu, kwa sababu hamna damu katika

mboga nyekundu." Kwa hiyo hamna aina yoyote ya Uzima ndani yao ili kupokea, kwa hiyo hauwezi kupokelewa.

59 Hiyo ndiyo sababu Mafarisayo walimtazama Yesu usoni moja kwa moja na kumuita "Belzebuli," kwa maana hakikuweko kitu ndani yao cha kumpokea. "Bali wote alionipa Baba," Yeye alisema, "watanijia mimi," Pana—pana njia ambayo itatolewa.

60 Unaweza wakati mwingine kuwaeleza watu barabani habari za Bwana, wakakuchekelea kwa dharau. Vema, inatupasa kufanya hayo hata hivyo. Bali sikiliza, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa kwanza na Baba Yangu." Inampasa Mungu kuvuta kwanza. Inapasa pawepo Uzima. "Na wote Alionipa Mimi watakuja Kwangu."

61 Ameweka mlango kwa wale wanaotaka kukombolewa. Aliweka mlango kwa wale waliotaka kuponywa. Ndipo kwa kufanya hayo akawa mwingi wa rehema, kama ambavyo Amekuwa mwingi wa rehema siku zote. Sharti iwe hivyo, kama ukikataa Hili, hakuna kitakachobakia isipokuwa Hukumu. Kwa sababu ni lazima dhambi ihukumiwe.

62 Farao alipoingia ba—baharini kama mwigaji, alidhania angaliingia kama Musa alivyofanya. Musa pamoja na jeshi lake, na Farao na jeshi lake wote pamoja walionekana iliwapasa kuangamia baharini. Bali Mungu, aliye mwingi wa rehema, akafanya mlango wa kutokea kwa ajili ya wana wa Waebrania, (kwa nini?) Kwa sababu walikuwa wakitekeleza wajibu wao, walikuwa wakifuata Neno.

63 Sasa hiyo ndiyo njia pekee ya kupata rehema, ni kufuata maagizo tuliyoamrishwa na Mungu tuyafuate. Hiyo ndiyo njia pekee Anayoweza kuonyesha kwayo rehema, ni tunapofuata aliyoagiza tutende.

64 Kama tulivyojadiliana kidogo si muda mrefu uliopita, na mhudumu mmoja wa kanisa aliyesema mimi nilikuwa nafundisha fundisho la kimitume siku hizi. Naamini nilieleza hayo siku moja au mbili zilizopita, au wakati fulani, jinsi alivyosema "Wewe unajaribu kuingiza fundisho la kimitume katika kizazi hiki." Akasema, "Zamani za kimitume zilikoma baada ya mitume."

Na mimi nikamuuliza, "Vema, je, wewe unaamini Neno?"

Akasema, "Ndiyo."

65 Nikasema, "Ufunuo 22:18 unasema hivi, 'Mtu yeyote akiondoa Neno moja katika Hiki, ama atakayeongeza neno moja katika Hiki,' si maneno mawili hivi; Neno moja, kuondoa Neno moja."

Akasema, "Ninaamini hayo."

66 Nikasema, "Basi naweza kukuambia ambapo zamani za kimitume zilipotolewa, baraka za Kimitume zilipotolewa kwa Kanisa; hebu niambie ambapo Mungu aliziondoa kanisani,

kwa Neno. Huwezi kufanya hivyo; hakuna." Nikasema, "Basi kumbuka ya kwamba, ile siku ya Pentekoste, Petro, ndiye aliye—aliyetangaza kuanza kwa zamani za kimitume. Na akawaambia wote, 'Tubuni mkabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.'"

67 Sasa kama unataka kusikiliza mlio wa kuku za kidhehebu, na kuishi humo katika mambo ya ulimwengu, hiyo itaonyesha kuna kasoro fulani. Maana hilo ndilo Neno. "Atakaye na aje," na iwapo unayo nia, itakupasa uje. Bali kama huna nia, basi uko katika hali ya kuhuzunisha. Lakini kama unayo nia ya kuja, njoo ufuate utaratibu wake Mungu!

68 Naye hakosi kutimiza aliyoahidi. Nilikuwa kijana, sasa ni mzee, nami sijamwona akishindwa katika Neno Lake. Haiwezekani kwa hali yoyote akose kutimiza. Hawezi kushindwa. Mungu hashindwi. Haiwezekani Mungu ashindwe, na awe bado ni Mungu. Yeye hana budi kufanya hivyo.

69 Sasa, jeshi la Farao lilijaribu kuiga, kwa kuwa halikuwa limeitwa nalo halikuwa na ule Uzima. Katika ile. . . Farao hakupewa ile ahadi. Hakuahidiwa ile nchi ya ahadi.

70 Na mwigaji anayejaribu kumfuata mwamini wa kweli aliyeitiwa hayo, huyafanyia dhihaka tu. Hiyo ndiyo shida ya mipango yetu ya dini siku hizi. Kuna watu wengi sana wanaojaribu kumwiga Roho Mtakatifu. Wengi sana wanajaribu kuiga ubatizo, wengi sana wanajaribu kuiga zamani za kimitume. Ni ya waamini na kwa ajili yao tu. Mungu amefanya mlango, ni mwingi wa rehema, ili watoto Wake wasiangamie. Amefanya mlango kwa ajili yao.

71 Sasa, Farao alijaribu kuwafuata, akazama katika maji yale yale yalioyomuokoa Musa na kundi lake. Sasa, Musa hakuzama, kwa sababu Mungu ni mwingi wa rehema kwa hao wanaoifuata njia aliyoweka tayari. Amina.

72 Je mnaweza kuona ninayomaanisha? Ya kwamba usiku wa leo wale ambao hawaamini katika uponyaji wa Kiungu, watu wasioamini ubatizo wa Roho Mtakatifu, watawezaje kupokea chochote? Mungu ni mwingi wa Rehema kwa wale wanaomfuata; siyo kufuata kanuni za dini, bali wamfuatao Mungu.

73 Mungu ni Neno, Nalo lilifanyika mwili na kukaa kwetu, naam, ili aweze kuleta yale mawazo mengine ya Mungu. Ule mwili, Yesu, ulikuwa mwili wa Mungu, wazo. Musa alimwona upande wake wa nyuma, alipokuwa akipita; hakuna mtu aliyekuwa amemuona uso Wake. Bali sasa tunamwona, tumemtazama Yeye, tukamwona kama dhabihu. Sasa, mnaona, Yeye alikuwa ni wazo la Mungu, katika kudhihirishwa Kwake, lile Neno. Hivyo ndivyo alivyokuwa.

74 Na mwamini yeyote anapokuja kwa Mungu anakuwa wazo la Mungu la Neno Lake, yeye anatumiwa kudhihirisha Neno lililoahidiwa kwa wakati huo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mungu, aliye mwingi wa rehema, hajatuacha bado bila ushuhuda. Yeye ni mwingi wa rehema.

75 Tunaona ya kwamba Mungu alimrehemu sana hasa Musa kule kwenye bahari ya chumvi, kule kwenye Bahari ya Sham, hasa. Ndipo aliposema hapa, katika Kutoka 19:4, Yeye alisema, "Niliwachukua ninyi juu ya mbawa za tai, nikawaleta ninyi Kwangu. Niliwachukua wao juu ya mbawa za tai na kuwaleteni Kwangu!" Kulikuwako na watu wengine katikati ya bahari kule, pia, wakijaribu kuiga. Bali nini? "Aliwachukua juu ya mbawa za tai."

76 Naam Mungu daima anawalinganisha manabii Wake na tai. Na ilikuwa nini? Musa alikuwa mjumbe Wake. Nao walikuwa wakimfuata Musa, na hizo ndizo zilizokuwa mbawa za tai walizobebwa juu yake, kwa maana alichukua ujumbe wa Mungu. Na wale watu walifuata hilo. Walikuwa wanamfuata Mungu walipomfuata Musa mwenye ujumbe wake wa ukombozi. Na Biblia inasema kwamba, "Yeye, wao hawakuangamia pamoja na wale ambao hawakuamini." Kwa maana, Mungu alikuwa mwingi wa rehema kwao, kwa sababu walikuwa wakifuata amri Zake. Mungu anatutaka tufuate amri Zake.

77 Tungesema yale yale kuhusu Kora na Dathani na kikundi chao cha watu wasioamini, walipojaribu kuiga. Walijaribu kuiga kitu fulani katika mpango wa Mungu. Hawakutaka mpango wa mtu mmoja. Hawakutaka hayo. Iliwapasa wapate jambo la kutenda. Kora alisema, "Mbona, kuna watu watakatifu kuliko wewe, Musa. Unajifanya kama kwamba wewe tu ndiye pwani kwenye . . . au ndiwe pekee kijiwe katika pwani, hasa." Akasema, "Mimi—Mimi . . . haukupaswa kufanya hivyo. Na kuna watu wengine hapa."

78 Naye Musa alijua ilimpasa kuwachukua hao watoto na kuwaingiza kwenye nchi ya ahadi, kwa sababu ile ahadi ni yeye alipewa. Naye alipaswa kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi.

79 Na siku hizi Roho Mtakatifu yupo hapa kudhihirisha Neno la Mungu, na hilo ndilo lile bawa la tai ambamo tunapaswa kujificha; si kwa theolojia iliyoundwa na binadamu. Bali inatupasa kuendea kwenye mabawa ya tai; ile nchi ya ahadi.

80 Nao hapa walikuwa wakienda kuleta kundi la kuku nje kule, Korah akadhani, mnajua, kuja huku na kuigiza hili, huyu tai. Na walipotenda hayo, Mungu akasema, "Jitengeni nao," na akaumeza ulimwengu. Angaliweza kumeza sehemu yote ile, na viumbe vyote, lakini Mungu alikuwa mwingi wa rehema kwa wale wanaojaribu kufuta Neno Lake. Daima Mungu ni mwingi wa rehema. Wengi wao walikuja upande wa Musa, naye Mungu

akafunua nchi na kuwameza wasioamini. Yeye a—asiyeamini ataangamia kila wakati.

81 Wale ambao hawakuamini, ingawa walitoka na kutembea kwa kitambo kidogo, bali wao, Yesu alisema, "Hao, kila mmoja wao, amekufa." Na *mauti* ni "kuangamia." Wamekufa. Waza juu ya hayo tu. Walitoka wakaona miujiza ya Mungu, wakauona mkono mkuu wa Mungu, wakafurahia mana; na kuenda kule na kumsikiliza mtu anayeitwa Balaamu, aliyepotosha njia za Mungu, kwa mafundisho yake yaliyolipinga Neno, "Sisi sote ni ndugu, kwa hiyo na tuwe pamoja."

82 Huo ni mpango mwingine wa Balaamu unaoinuka, siku hizi, "Sote na tuwe pamoja." Haitawezekana. Na tuende pamoja na yule Tai, Yehova Tai. Ninyi ni wana tai.

83 Watatu tu ndio waliookolewa kutoka katika lile kundi zima; Musa, Kalebu, na Yoshua. Wengine wao waliangamizwa jangwani; Yesu alisema hivyo, Injili ya Yohana mlango wa 6. Mungu, kwa rehema, hangewaacha waangamie, kwa sababu, pamoja na wale wasioamini. Wote walifia pale pale jangwani, nao wamekufa. Mungu alimwokoa Musa pamoja na wale tai waamini, kwa maana waliheshimu Neno Lake.

84 Na Leo, rafiki, njia tu tunayoweza kupata heri kwa Mungu; Mungu ni mwingi wa rehema, leo, bali inatupasa tuheshimu aliyosema juu yake. Huwezi kupokea alichosema mtu mwingine. Inakupasa kupokea aliyosema Mungu. Yeye alisema, "Na neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu kweli."

85 Leo tunaambiwa kwamba, "Yote yanayokupasa kufanya," mahali pengi, "ni kujiunga na kanisa, kufuata kanuni za imani, ama kitu kama hicho; ama kuomba dua, ama kuandikwa jina lako kwenye kitabu, ama ukanyunyiziwa maji au kubatizwa kwa njia fulani, au kitu kama hicho. Hayo ndiyo unayopaswa kufanya." Lakini hayo ni makosa.

86 Ili kuwa tai wa Mungu, inakupasa kufuata Neno, siku kwa siku. Inakupasa kuendelea kula Neno.

87 Basi twawaona baada ya hayo wakinung'unika tena, imani zao zimedhoofika hata baada ya Mungu kuwaonyesha rehema. Na tunawapata wakimnug'unikia Mungu, na walipofanya hayo walikuwa wanakufa kwa kuumwa na nyoka. Bila shaka walistahili hayo. Hakika walistahili. Yeyote ambaye angekosa Neno la Mungu na kutenda mambo hayo waliyotenda, walistahili kufa. Kila mmoja wao aliyetamani, alistahili kufa jangwani.

88 Bali walipokuwa hawawezi kabisa na hata Daktari Musa na wengine wao hawangeliweza neno, nao walikuwa wakifariki kwa maelfu; bali Mungu, mwingi wa rehema, alifanya mlango wa kutokea kwa wale ambao wangemwamini. Alitengeneza dawa Yake kwa kuinua nyoka wa shaba. Mungu kwa utajiri

Wake...Mungu alifanya mlango wa kutokea ili watoto Wake wanaomwamini wapate kuponywa.

89 Mungu hushughulikia kila jambo baya, yote unayoyawazia. Kwa kila hatua maishani, Mungu anajishughulisha na wewe. Wewe u mtoto Wake, yeye ni mwingi wa rehema. Anataka kukusaidia.

90 Wale watu walitenda dhambi baadaye, kwa kuchukua kitu kile kile ambacho Mungu aliwafanyia upatanisho, kwa nyoka wa shaba ambaye aliwakilisha dhambi ambayo tayari imekwishahukumiwa, nao wakakifanya kipawa hiki ibada ya sanamu. Na kwa hiyo wakafanya dhambi tena. "Mungu hatashiriki utukufu Wake na mtu yeyote." Kwa hiyo hatutaweza kuwa na miungu wawili, watatu, wanne, kuna Mungu mmoja pekee. Hatashiriki utukufu Wake pamoja na chochote kile. Yeye ndiye Mungu peke yake, mwaona; kama vile makafiri walivyo na miungu wengi. Tuna Mungu mmoja, naye hatashiriki utukufu Wake na yeyote yule, wala hataacha chochote kiabudiwe mbele Zake. Ingawa alikuwa amefanya upatanisho kwa ajili ya watu, na ilikuwa Neno la Mungu, ilikuwa sawa; bali walipotengeneza sanamu, ndipo walipoingia kwenye shida.

91 Naam, hilo ndilo jambo lile lile lililotendeka katika nyakati zetu za kanisa. Mungu alitutumia ujumbe wa Martin Luther na ujumbe wake, John Wesley, ujumbe wa Kipentekoste, bali tulifanya nini nao? Jambo lile lile walilotenda na yule nyoka wa shaba, tukauabudu, "Mimi ni mshiriki wa *hili,* nami ni wa *lile.*" Waona unahusika na kitu bila ule uaminifu wa kweli uliohusishwa na ibada halisi ya Neno.

92 Nini ilitendeka? Biblia, tunaambiwa na Biblia, ya kwamba, "Nabii aliichukua sanamu hiyo na kuiharibu." Haleluya!

93 Tunachotaka siku hizi ni nabii ambaye ataangamiza sanamu ya madhehebu, wanaofikiri ya kwamba watakwenda Mbinguni kutokana na kuwemo katika kanuni fulani za imani au dhehebu; hii inapasa kuangamizwa na kuchomwa moto, na kutupwa mbali. Mungu amejaa rehema. Yeye ni mwingi wa rehema. Katika siku ambazo tungekuwa katika mchafuko huo wa giza kule, bali Mungu, mwingi wa rehema, ametutumia Roho Mtakatifu wa kweli hasa, akifasiri Yeye Mwenyewe papa hapa katika jengo hili kila siku. Mungu, mwingi wa rehema, jinsi tunavyomwona kuwa wa ajabu! Naam, bwana.

94 Yote waliyodhani wangefanya ilikuwa tu kwenda kwa huyu nyoka, ama hiki kitu kidogo Mungu alichofanya pale, alichomwamuru Musa kutengeneza na kukitundika mtini. Nao wangaliponywa bila uaminifu wowote, walisimama tu na kutazama. Nao wakaanza kuiabudu, naye Mungu akamtuma nabii kuingamiza.

95 Sasa, wale waliokataa kuitazama ile nyoka, jangwani, waliangamia. Basi Mungu huweka njia, bali ukikataa

kuitazama, iwapo utaketi barabarani, iwapo utashikilia kanuni fulani ya dini, na kukataa kulitazama Neno moja kwa moja na kuona kama ni kweli au la; wote waliokataa kutazama, waliangamizwa. Na Mungu ni Mungu asiyebadilika. Wote waliokataa kutazama waliangamizwa. Vivyo hivyo leo, kitu kile kile.

96 Ndipo watu wakatenda dhambi baadaye, na wamefanya hivyo kila mara, na kufanya sanamu kutokana—kutokana nayo, na kuifanya a—a—a . . . kujaribu kuponywa bila uaminifu, nao "ni washiriki wa kitu fulani," na tunavyofanya siku hizi. Na sasa basi tunaona tofauti yake, ilikuwa ya kwamba Mungu . . .

97 Ilikuwa upatanisho mzuri na ishara nzuri ya wakati ule. Wakati huo, ilikuwa sawa. Bali ilikuwa tu kwa wakati huo, kwa safari hiyo. Hayo ndiyo yote itatosheleza, *safari hiyo*.

98 Na ujumbe ambao Martin Luther aliuleta, wa kuhesabiwa haki, ulifaa kwa wakati wa Luther. Ukakoma hapo.

99 Kutakaswa kulikuwa sawa wakati wa Wesley. Kukakoma hapo.

100 Ndipo tunaingia wakati wa Pentekoste. Na kurejeshwa kwa zile karama kulikuwa jambo jema mno, ilikuwa sawa kwa kizazi hicho, bali tunaenda mbele zaidi ya hapo sasa. Tumepita hayo, kama tulivyo na uhakika kuna dunia. Inatupasa tuende mbele zaidi ya kitu hiki, maana tuliyofanya juu ya jambo hili ni kama na hao wengine walivyofanya huko nyuma, yaani kufanya sanamu toka kwake. "Mimi ni mshiriki wa mpango huu wake, mimi ni mshiriki wa mpango *ule* wake."

101 Mungu atamtuma mtu atakayevunja kitu hicho na kukipasua vipande vipande, na kulithibitisha Neno Lake, Neno zima. Tazama. Mungu atukuzwe! Sasa tunaona kuwa hayo ni kweli? Mungu, mwingi wa rehema Zake!

102 Ndipo yule nabii alipoangamiza hii, aliwaacha bila ishara yoyote ya uponyaji, ya upatanisho, kwa sababu sanamu yao iliangamizwa. Bali Mungu, mwingi wa rehema akawafanyia nyingine. Na alifanyaje hayo? Aliyatibua maji kwenye birika hekaluni, wengi walikuja na kuponywa kwa kuingia majini. Yesu alikuja katika kidimbwi hiki na kumwona mtu aliyekuwa amelala pale miaka mingi akisubiri maji yatirehema! Mwaona Mungu, mwingi wa rehema! Ijapokuwa walikuwa wamejifanyia sanamu, na nabii alikuwa ameivunjavunja. Mungu aliwawekea njia nyingine, kwa sababu Yeye ni mwingi wa rehema. Anataka waponywe, Naye anawatayarishia njia ya uponyaji.

103 Basi, hayo yaliendelea, ulimwengu uliendelea kuwa na dhambi zaidi na zaidi kila wakati. Na mwishowe ulimwengu uliingia dhambini mno, hata Mungu angaliweza kuuangamiza. Alisema katika Malaki 4, "Nisije nikaipiga dunia kwa laana." Angalitenda hivyo; ndilo tu swali.

104 Bali Mungu, mwingi wa rehema, akamtuma Mwokozi, Yesu Kristo. Naye alimtuma Yesu Kristo awe Mwokozi na Mponyaji. Kwa maana Yeye alisema, “Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa,” kwa kusudi lile lile. Yeye, aliye huo upatanisho, huo ndio tunaoweza kudai, si kingine ila huo upatanisho. Kile alichonunua Yesu kwa Damu Yake, ndicho tunachoweza kudai. Na Biblia yasema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” Hayo ndiyo tunayoweza kudai, kwa sababu hayo ndiyo ule upatanisho, ambao tunautumainia, uliowekwa kwa ajili yetu. Mungu, mwingi wa rehema!

105 Huu ulikuwa upatanisho wa Milele, kwa sababu Alikuja Yeye Mwenyewe. Mungu alikuja Mwenyewe, kwa mfano wa mwili wenye dhambi, kufanya u—u—u—upatanisho wa Milele; na akateseka mwilini, na kuufanya upatanisho; na akarudi tena akiwa Roho Mtakatifu, ili kuthibitisha huo upatanisho. Ambao sio nyoka wa shaba na wala sio maji yaliyotibuliwa ingeweza kufanya hayo, hayo yalielekeza kwenye ule Ukombozi mkamilifu. Ni Mungu, mwingi wa rehema Zake, aliyefanya hayo.

106 Basi, leo, katika siku tunazoishi, tumepitia hizi nyakati za kanisa na kuelezea kila kitu mbali na Hilo. Wanatheolojia wa siku hizi wamepoteza upande huo wake. Wamelieleza vingine, kwa ajili ya siku zingine, wakati mwingine, mengineyo, mbali sana, wakati mrefu sana uliopita. Na uponyaji wa Kiungu ulikuwa karibu kuondolewa kabisa, vigumu kupata mtu yeyote aliyeuamini. Waliufanyia mzaha. Si zaidi hata ya miaka ishirini iliyopita walikuwa wakiufanyia mzaha. Wapentekoste walikuwa karibu kabisa kuuacha. Walivanzisha siku za mwanzoni, bali wakauacha.

107 Tazama walivyofanya. Sasa wameingilia upotovu wa kidhehebu, kila mmoja akikimbilia kuunda kanuni za kidini, na kadhalika. Ijapokuwa, badala ya kukubali Nuru, wakati Nuru ilipoingia; walijiundia dhehebu na wakajitungia kanuni za imani, na kila mmoja akija na kujitungia mafundisho yake mwenyewe na kudumu katika hayo mafundisho. Ndipo wakachukuliwa mbali sana hata Roho Mtakatifu hakuweza tena kuingia kanisani. Wakawa kama sanamu nyingine tu, kama nyoka wa shaba, ikawa ni—ni ibada ya sanamu. Kila mtu akasema, “Mimi ni mshiriki wa *hili*, nami ni mshiriki wa *lile*.” Ilikuwa ni ibada ya sanamu. Tuko kwenye vurugu kubwa vipi, wakati huu wa mwisho.

108 Bali Mungu, mwingi wa rehema Zake, ametutumia Roho Mtakatifu, na kudhihirisha Neno Lake usiku huu kama alivyoahidi angefanya. Mungu aliahidi ya kwamba angefanya mambo haya. Tazama aliyoyafanya!

109 Tazama aliyoyafanya, vile tunavyoweza kuona jinsi Alivyoahidi katika kila kizazi jambo fulani lingetokea. Na tumethibitisha kuwa kila kitu kimetokea vile vile kama alivyosema angefanya, kwa sababu yeye ni mwingi wa rehema Zake, na daima rehema Zake ni kutimiza kila Neno aliloahidi. Imempasa kufanya hivyo kila mara ili adumu kuwa Mungu. Daima amefanya hivyo, na Neno Lake siku zote katika majira Aliyoyaamuru. Mbegu Yake ambayo amepanda duniani. Alifanyaje? Aliiweka hapa katika Neno, na hiyo ni mbegu. Na kila wakati kizazi kinapokuja, mbegu ya kizazi hicho hupevuka, ndipo matengenezo hutokea. Na yeye aliahidi hivyo, na ndivyo inavyokuwa.

110 Naam hatukustahili vitu hivi. Hatukustahili baraka hizi za Mungu, kwa sababu tulikuwa tumefuata vitu vya ulimwengu, na kuingia katika kosa la Kaini. Kaini, alijenga madhabahu nzuri, kanisa zuri, na kupamba kwa maua, akidhani kuwa hivyo ndivyo ilivyopasa hasa, "Ni kichala cha matofaa, ama mapera, ama makongomanga, au vyovyote ilivyokuwa," ambayo baba yake na mama yake walikula katika bustani ya Edeni, ikawafanya kufukuzwa. Ndipo akamtolea Mungu hayo, Naye Mungu akayakataa.

111 "Bali Habili kwa imani alimtolea Mungu dhabihu bora kuliko Kaini."

112 Na, siku hizi, Biblia inasema katika Yuda, ya kwamba, "Walikwenda katika njia ya Kaini; nao wameangamia katika maasi ya Kora." Mwaona, "kwenda katika njia ya Kaini," kujenga madhabahu, kujenga makanisa, madhehebu, wakiyapamba kwa maua, makanisa makubwa, washirika wengi kuliko wengine wao; wakipokea vitu, chochote kinachokuja, na vingine vya kurukaruka, na kushikana mikono, au kubatizwa namna fulani, au kunena kwa lugha, au kukimbia kwenye sakafu na kuandikwa jina kitabuni. Naam. Na kisha wanaugeukia mbali Ukweli halisi unaohubiriwa, na kuukana. Itawezekanaje? Tazama vurugu kubwa tuliyoko ndani yake! Tazama.

113 Nayo Biblia ilisema, "Walikwenda njia ya Balaamu, na kuangamia katika maasi ya Kora." Kuangamia katika maasi! Je maasi ya Kora yalikuwa nini? "Je, unadhani wewe tu ndiye mtu aliye mtakatifu peke yako? Kwa nini, wa Mungu . . . Sisi sote tu watakatifu. Kanisa lote ndivyo lilivyo. Kila . . . Sote tukusanyike, ndivyo inavyotupasa kuwa." Hivyo ndivyo walivyoangamia, katika hilo. Na tulistahili hayo kabisa. Tulistahili hayo.

114 Bali Mungu, mwingi wa rehema, ametuvuta kututoa kwenye hayo machafuko na kuturuhusu kuyaona mambo haya kabla ya maangamizi kutokea. Mwingi wa rehema Zake, na akatutumia tena uamsho wa uponyaji wa Kiungu, na kuturejeshea tena Uweza wa Mungu. Kufuatana na historia, hakuna uamsho unaopita miaka mitatu. Huu uamsho umeendelea kwa miaka

kumi na mitano, umekuwa ukiwasha mioto kuzunguka ulimwengu. Kwa nini, kwa sababu tulistahili? Mungu, mwingi wa rehema Zake, si kwa kuwa tulipenda hayo, au kwa sababu tulistahili, hasa. Hebu fikiri tu yale yaliyotendwa!

115 Nawaza juu ya mmoja wa dada zenu hapa papa Phoenix, ambaye wengi wenu mnamfahamu, Bibi Hattie Waldrop, yeye alikuwa mgonjwa wa kansa ya moyo. Naye alikuwa katika msitari wa maombi hapa wakati mimi na Ndugu Moore tulipokuwa hapa kwa mara ya kwanza, kama miaka kumi na tano, kumi na nane iliyopita. Yeye alikuwa akifa, kwa kansa ya moyo, na ilimpasa kufa wakati mwingi uliopita. Bali Mungu, mwingi wa rehema, akamtumia Uwezo Wake. Naye akamuokoa maisha yake, naye yuaishi leo. Mungu mwingi wa rehema!

116 Mjumbe Upshaw, mtu mkuu sana. Nadhani alikuwa rais, ama vinginevyo wa—wa Babtisti, Southern Babtist Convention, wakati mmoja, au makamu wa rais au kitu kama hicho. Alikuwa amefanya yote. Alikuwa mtu mwema. Alitenda yote aliyoweza kutenda. Yeye alikuwa amemwendea kila daktari. Hakuna aliyeweza kumfanyia lolote. Hakuwa na matumaini tena. Watumishi walikuwa wamemwombea. Alikuwa amemiminiwa galoni moja ya mafuta, upako kichwani mwake na watumishi mbali mbali kila mahali.

117 Na usiku mmoja, Los Angeles, California, nikipanda kwenye mimbara, nilitazama kundi la magari ya kusukumwa, yapata mara mbili au tatu ya hao wanaoketi hapa yote juu chini roshani, huku na huko. Na ndipo hapo palikuwapo kijitanda chenye mtoto mchanga mweusi, mtoto Mnegro, na—na mama yake alikuwa ameketi karibu naye. Na ndugu yangu alikuwa anautayarisha msitari wa maombi.

118 Nilikuwa nikitazama, bila kujua yaliyokuwa yakitendeka. Nilimwona daktari, mwenye miwani ya galili la kobe, akimpasua msichana mchanga wa kinegro, kwa ugonjwa wa koo, naye alikuwa amepooza. Nami nikatazama huku na huko, nikawaza, "Yu wapi mtoto yule?" Singelimwona.

119 Punde si punde, kule chini, bila tumaini, mtoto msichana mwenye umri wa miaka saba au minane, ambaye ni wa kupooza maisha yake yote yaliyobakia. Naye mama yake amepiga magoti, akimwombea. Ndipo nikasema, "Daktari huyu alimfanyia mtoto wako msichana upasuaji," nikaelezea.

Yeye kasema, "Hiyo ni kweli, bwana."

120 Ndipo akamleta mtoto yule jukwaani. Wakamwambia asifanye hivyo. Wakajaribu kumnyamazisha. Mara walifaulu kumnyamazisha. Nikawaza, "Vema, tutapata nafasi ya kumwombea." Katika dakika chache. . . Labda watu walioko hapa mlikuweko kule usiku huo.

121 Nami nilikuwa nikitazama kule kwenye umati, nikamwona yule msichana kama kwenye—kwenye barabara ndogo

iliyosonga, amembeba mtoto wa bandia mikononi mwake, akimbembeza. Si hoja daktari alikuwa amesema mara ngapi kuwa mtoto huyo angalipooza maishani mwake mwote; Mungu, mwingi wa rehema, alimshusha Roho Mtakatifu, kwa ono, na yule mtoto msichana akainuka kutoka pale, naye pamoja na mama yake wakashikana mikono na kutembea kwenye roshani, wakimsifu Mungu.

122 Kule nyuma kabisa aliketi mzee mmoja, Mjumbe wa Bunge Upshaw, wengi wenu wanajua ushuhuda wake. Alikuwa mtu mwema, alijaribu maishani mwake mwote, mgonjwa kwenye kiti cha kusukumia wagonjwa muda wa miaka sitini na sita, akisukumwa kitandani; akiwa na mkongojo chini ya mikono yake, aliyotembelea, hangeweza kutembea kwa kawaida kamwe. Naye aliketi pale, akitazama hayo. Na mara nikatazama na kuona ono. Hapa yuaja, akishuka kupitia juu ya umati ule, huku ameinamisha kichwa chake, angalitembea vizuri tu tena kama mtu yeyote yule. Sikujua yule mtu alikuwa nani.

123 Nikasema, "Pana mtu mashuhuri aliyeketi nyuma kule. Alianguka kutoka garini alipokuwa mvulana mdogo, akaangukia chuma ya kufungia majani ya ngombe, akaumia mgongo wake. Walitoboa mashimo sakafuni, kuzuia msukosuko, watu walipotembea, mgongo wake usiumizwe." Nikasema, "Anakuwa mtu mashuhuri, na anazidi kuwa mkuu. Yeye anaketi kwenye mviringo mkubwa katika Ikulu ya Marekani."

124 Na mtu huyu akaja na kuniambia, akisema, "Yule ni Mbunge Upshaw. Je, uliwahi kumsikia?"

Nikasema, "Sijawahi kumsikia."

125 Ndipo akampelekea kipaza sauti kule nyuma na walikuwa wakiongea, huku na kule.

126 Ndipo nikaanza kutazama huku na huko, nikamwona yule mzee mbunge akija akitembea kunijia, katika maono, akiwa mzima kabisa kama ambaye hakuwahi kuwa na ulemavu. Mungu, mwingi wa rehema, akamvuta kutoka kwenye kile kiti cha kusukumia wagonjwa, na akatembea bila mkongojo hadi siku aliyokufa. Mungu mwingi wa rehema! Madaktari waliposhindwa, sayansi iliposhindwa na kila kitu kilishindwa, Mungu alikuwa mwingi wa rehema kwa Mbunge Upshaw.

127 Najifikiria mwenyewe. Nilipokuwa mvulana mdogo, nakumbuka kama . . . watu wanavyoniita siku hizi "mchukia wanawake." Sababu yake ni kwamba, niliona utovu wa maadili mwingi sana miongoni mwa wanawake nilipokuwa mtoto. Nikawachukia. Lakini sivyo nilivyo sasa, najua wako walio wema miongoni mwao. Lakini nakumbuka mambo yalivyokuwa mabaya, uovu mwingi mno. Ndipo nikawaza, "Jamani, sita—sitaweza kuchangamana na watu wengine. Sina elimu, na wala sitaipata."

128 Nilipokuwa nikiketi pale nikiwa mtoto mdogo, sikuwa hata na shati, huku koti langu limefungwa *hivi* kwa pini, huku kukiwa na joto jingi. Naye mwalimu akasema, "William, je, husikii joto kwa kuvaa hilo koti?"

129 Nikasema, "Sivyo, mama, mimi nasikia baridi kidogo." Naye akanilazimisha kwenda kwenye jiko na kuongeza kuni zaidi, jikoni, na nilikuwa karibu kuchomeka. Nami si—sikuwa na shati majira hayo yote.

130 Ndipo nikawaza, "Iwapo ningalipata fedha, wakati mmoja nikipata kidogo ningenunua bunduki aina ya thelathini—thelathini, ningekuja huku Magharibi na kuishi huku na kuwinda, maisha yangu yote." Sikutaka uhusiano wowote na watu. Nikae tu mbali nao, kwa sababu hawakunitaka, na—nikae mbali nao.

131 Na ndipo kila nilipokwenda mjini kuongea na yeyote, watu wengine niliowajua kwenye njia za mji. Ningesema, "U hali gani, Yohana, Jim! Uhali gani?"

"Lo, sijambo."

132 Mnaona, hawakupenda kusema nami, hawakutaka uhusiano wowote na mimi, kwa maana baba yangu na wengineo walikuwa wakitengeneza pombe. Nami—nami sikuwa nikifanya hayo. Si kwamba nilikuwa nimefanya lolote. Na ningelikwisha kuwa mtu wa aina hiyo.

133 Ndipo nilimwambia mke wangu, si muda mrefu uliopita, "Ukuta wangu umejaa bunduki bora sana nikilinganisha na zilizoko madukani." Jamani, nami nafikiri juu ya zile nguo chafu na zilizochakaa. Leo nina suti mbili ama tatu nzuri. Na bila marafiki? Inanibidi kujificha jangwani, kuwakimbia watu. Imekuwaje, ni kwa sababu ya hali yangu, ni kwa sababu ya elimu yangu? Sivyo. Mungu, mwingi wa rehema, aliniona katika hali hiyo na kuniokoa mimi.

134 Nakumbuka nilipokuwa nikiongozwa kwa kushikwa mkono, kama kipofu. Sikuwa ninaweza kuona. Kila kitu mbele yangu kilikuwa na kiwi; Ningekuwa kipofu maishani yangu yote. Bali Mungu, mwingi wa rehema, alinirudishia kuona kwangu. Nina umri wa miaka hamsini na mitano, na macho yangu bado yanaona vizuri. Mungu, mwingi wa rehema, ndilo ninaloweza tu kusema.

135 Wakati mmoja kanisa halikuwa na njia iliyotolewa ya uponyaji. Walikuwa nayo lakini wakaiacha. Lakini Mungu, mwingi wa rehema, akawatumia karama ya uponyaji wa kiungu. Huyo ni Roho Mtakatifu miongoni mwetu, akithibitisha Neno kwa ishara zilizofuata. Mungu mwingi wa rehema!

136 Nina kurasa mbili ama tatu za maandishi haya, bali sitajaribu kuyagusia, kwa sababu nina—ninaona wakati

umewadia wa kuanza msitari wa maombi. Lakini Mungu mwingi wa rehema!

137 Wengi wenu mlioko hapa usiku huu, madaktari wamewakataa. Kuna watu hapa walioketi kwenye magari ya kusukumia wagonjwa, huenda wasitoke humo tena. Hawatatoka humo. Baadhi yao walipooza kwa namna mbalimbali, wao (hawangeweza kamwe) hawangeweza kutoka humo, hakuna njia kwao kutoka katika hayo. Lakini Mungu, mwingi wa rehema Zake, ametupa upatanisho. Usiukatae. Upokee. Kuna mtu pale mwenye ugonjwa wa moyo, kuna watu walio na kansa, ambayo madakatari hawawezi neno. Hamna tumaini, msaada, humu duniani.

138 Bali Mungu, mwingi wa rehema Zake, ametutumia Roho Mtakatifu, na papa hapa sasa kuthibitisha Neno, kuthibitisha kwamba ni Yeye Yule jana, leo na hata milele. Kwa sababu tunastahili? Kwa sababu Mungu ni mwingi wa rehema! Amina. Sasa huyu Ndiye, ndiye Mtu yule, ndiye Bwana Yesu. Yeye si mfu, Amefufuka kutoka kwa wafu, na Yu hai hata milele.

139 Yeye ni yeye yule, jana, leo na hata milele, bado ni mwingi wa rehema Zake kama alivyokuwa kwa yule mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu. Naye akapitia katikati ya makutano. Hapakuweko na matumaini kwake, madaktari walikuwa wamekwishafanya kila waliloweza. Alikuwa akitokwa na damu. Alikuwa anakufa. Na aligusa vazi la Bwana. Mungu, mwingi wa rehema, aligeuka na kumwambia hali yake. Naye aliponywa ugonjwa wa kutokwa na damu.

140 Kijana mwovu kahaba alikwenda kisimani siku moja, kuteka maji. Hana tumaini. Alikuwa ametengwa na mabikira, na majirani, maisha yake hayakuwa mema. Naye akawaza, “Ya nini kujaribu? Nimetengwa, hakuna kilichobaki kwangu.” Akatazama akisimama upande mmoja, ama akiketi karibu na kisima kile, na palikuwepo Mtu aliyeketi pale na kumwambia mambo yote aliyotenda, Mungu mwingi wa rehema Zake.

141 Mungu yule yule usiku huu bado ni mwingi tu wa rehema, na yuko tu vile Alivyokuwa siku hizo. Mungu mwingi . . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

142 Nafikiri tuna kadi mia mbili za maombi hapa, au wale tuliokwishawaita ni mia mbili. Tutawaita na kuwapanga mstarini. Tutawaombea.

143 Bali kabla hatujafanya hivyo huenda ikawa kuna wageni hapa, wangesema, “Acheni huo ushirikina wote?” Huu si ushirikina. Huu ni udhihirisho wa ahadi ya Mungu. Inategemea unachotazama. Hakuna mtu yeyote mwenye nguvu. Hakuna mtu yeyote mwenye uwezo. Lakini sisi tukiwa waaminio tunayo mamlaka; si uweza, bali mamlaka.

144 Mtu mmoja aliniuliza, muda mfupi uliopita, kasema, “Ndugu Branham, unaamini una uweza wa kufanya haya?”

145 Nikasema, “Sina uweza, hata kidogo, bali mamlaka.” Kila mwamini anayo. Ukikataa utabaki mahali ulipo. Lakini kama utakubali, utafanya mambo makuu sana, kwa maana Mungu ni mwingi wa rehema Zake.

146 Kwa mfano kijana polisi anayesimama kwenye barabara za mji, mavazi yake yakining’inia nusu nje, mwembamba sana. Kofia iliyovuta masikio yake chini. Naye atembea ambapo motakaa zinakuja barabarani mwendo wa maili hamsini kwa saa, mwendo wa nguvu za farasi mia tatu. Yeye hana hata nguvu ya kusimamisha angalau baisikeli. Naam. Bali mwache apige hiyo filimbi na kunyosha mkono wake, na utaona jinsi breki zitalia kweche kweche. Yeye hana uwezo, bali ana mamlaka. Mji mzima uko nyuma yake.

147 Na wakati mwanamume au mwanamke, si hoja uko katika hali gani, unayo mamlaka kutoka kwa Mungu, kwa ahadi, kwa sababu Yeye ni tajiri na ametuahidi kutufanyia mengi mno. “Kama ukiuambia mlima huu ‘Ng’oka’ na usione shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba hayo usemayo yametukia, yatakuwa yako.” Huna uweza wowote, bali unayo mamlaka.

148 Kumbukeni Yeye aliponiambia siku za nyuma akisema “Utaweza kufichua siri zilizoko mioyoni.” Kwa maana Yeye . . . Mnakumbuka hayo, wengi wenu watu wa Phoenix? Aliahidi. Anayoahidi, Yeye hutimiza.

149 Sasa kuna wengine wenu hapa wasiokuwa na kadi za maombi, bila shaka. Ni wangapi wagonjwa wasiokuwa na kadi za maombi, inueni mikono yenu? Kweli. Sawa. Basi kama unataka kujua, sio mamlaka . . . wala uwezo, bali mamlaka ya Neno, “Kazi nizifanyazo Mimi nanyi pia mtazifanya.”

150 Yesu aliahidi katika Luka 17:30, kuwa muda mfupi kabla ya Kurudi Kwake, ingekuwa kama siku za Nuhu, Musa . . . au Nuhu, “Wakati walipokuwa wakila na kunywa na kuolewa; na hawakujua hata siku ile Nuhu alipoingia katika safina.” Alisema kungekuwa na wakati huo. Ndipo pia akasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu,” akasema, “hii itatendeka siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu, atakapofunuliwa Mwana wa Adamu katika siku za mwisho.”

151 Sasa tazama jinsi Yeye, jinsi Mwana wa Adamu alivyojifunua Mwenyewe katika nafsi ya huyu Malaika, ambaye alikuwa ndiye Mwana wa Adamu. Hakika. Ibrahimu ndiye alimwita, “Elohim.” Alikuwa Mwana wa Adamu, aliyejifunua Mwenyewe kabla tu ulimwengu wa Mataifa kuchomwa moto. Yeye alifanya hivyo vipi? Kwa waamini. Kwa wajifanyao waamini, aliwatumia wahubiri wawili chini huko kuwahubiria. Bali kwa waamini halisi, akisimama mgongo Wake ukielekea hemani, naye akasema, “Ibrahimu.” Yeye alikuwa Abramu siku

ile . . . siku chache kabla ya hapo. Bali sasa yeye ni Ibrahimu "Yu wapi mke wako Sara?"

152 Akasema "Yumo hemani, nyuma Yako."

153 Akasema, "Nitatimiza ahadi Yangu kwako. Nitakurudia."

154 Lo, Ibrahimu alikuwa mwenye umri wa miaka mia moja, naye Sara alikuwa tisini; bali Mungu, mwingi wa rehema, akatimiza ahadi Yake. Ikamleta mwana, maana Mungu ni mwenye huruma, Naye amejaa rehema. Ni mwingi wa rehema. Hutimiza ahadi Yake.

155 Tazama, huku mgongo Wake umeelekezwa hemani, Sara akacheka na kusema, "Je mambo haya yatawezekanaje? Mimi ni mkongwe. Naweza kupata furaha pamoja na bwana wangu, kama mwanamke kijana aliyeolewa? Mbona, yeye ana umri wa miaka mia moja. Uhusiano wetu wa mume na mke ulikoma miaka mingi, mingi sana iliyopita. Hili litawezekanaje?" Ndipo akacheka juu ya jambo hili.

156 Na yule Malaika . . . yule Mwana wa Adamu huku mgongo Wake ukielekea kwe—kwenye hema, akasema, "Mbona Sara amecheka, akisema, 'mambo haya yatawezekanaje?'"

157 Ilikuwa nini? Yesu alisema 'katika Luka Mtakatifu 17:30' kuwa, "Katika siku kama ilivyokuwa katika siku za Lutu," hali ile ile, kabla ya ulimwengu wa Mataifa kuchomwa moto, Alisema, "Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe katika siku hiyo." Yeye aliahidi ya kwamba ahadi za Malaki 4 zitatimizwa. Ujumbe ungekuja ambao ungerudisha watu kwenye Ujumbe wa pentekoste ya kwanza, pamoja na baraka zile zile walizokuwa nazo katika siku ya . . . Ni nini? Ni tai mwenye mabawa mawili, Agano Jipya pamoja na Agano la Kale, kukusanya ahadi zake pamoja, za Mungu, kutimiza ahadi za Biblia ilivyosema kwamba zitakuwa. Amina.

158 Mungu, mwingi wa rehema, hangeliacha watu wake waingie katika haya madhehebu, "yaliyojitajirisha kwa vitu na mambo ya ulimwengu," wakati wa kanisa la Laodikia, bali angeweka mlango wa kutoka. Aminini hayo enyi watu. Mungu awabariki. Amina. Mungu mwingi wa rehema! Rehema za Mungu, hizo ndizo ninazozihitaji. Si haki Zake, si amri Zake; bali rehema Zake ndizo ninazoomba. Mungu anirehemu mimi. Sote tunajisikia hivyo.

159 Nilikuwa ninaagalia. Pana mwanamke mmoja mdogo ameketi pale mwisho wa kiti. Je, una kadi ya maombi kule, dada? Huna. Hebu nikuonyeshe Mungu ni mwingi wa rehema. Umekuwa mwenye wasiwasi juzi juzi, sivyo? Vibaya sana, na mambo yako yamekuwa mabaya zaidi. Sivyo? Hiyo ni sawa. Sasa yatabadilika. Mungu, mwingi wa rehema Zake, kwa kukuuliza kama ungaliweza kuamini haya. Sasa, huna kadi ya maombi, huna chochote; bali sasa hutaihitaji. Waona, umetunukiwa neema.

160 Pale mbele ameketi mtu mmoja mdogo, akiwa na . . . ameketi pale pale. Anaumwa uvimbe katika mwili wake. Umeingia pale majuzi tu, majuzi. Sivyo, bwana? Hiyo ni sawa. Hujui ni nini. Una hofu juu yake. Sawa. Ulisababishwa na chubuko, sivyo? Je una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi. Hutaihitaji. Mungu mwingi wa rehema Zake!

161 Jamani, ndugu, dada, mwamini Mungu! Usimtilie shaka. Mwamini Yeye! Naam.

162 Hapa ameketi mtu mwenye suti ya kijivujivu, amevaa miwani. Tazama huku, bwana. Je, unaamini? Mungu mwingi wa rehema Zake. Umeketi hapo ukiugua mishipa. Je unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya huo ugonjwa wa mshipa na kukufanya mzima? Uliyeketi pale pale mwisho wa kiti ukinitazama. Kama unaamini kwamba Mungu anaweza kukuponya huo mshipa, Mungu atakufanyia hayo iwapo utakubali hayo. Je, unaamini? Utakubali? Sawa. Unaweza kupokea kama utaamini tu, pokea rehema. Ndiyo, bwana.

163 Hapa yupo mwanamke aliyeketi humu, anaugua mzunguko wa damu mwilini mwake. Bali iwapo ataamini, Mungu atamponya, akiamini. Naamini hataweza kupokea, hakika. Umrehemu, ndilo ombi langu. Kama ninavyoona dhahiri mwanamke huyu ni . . . Bi. Riley, je unaamini kuwa Mungu anaweza kuponya huo mzunguko dhaifu? Kama utaweza, pokea! Amina. Amini tu. Mungu yu mwema, sivyo, Stella? Naam. Ndivyo. Sijamwona huyo mwanamke maishani mwangu. Bali, Mungu, kwa rehema Zake!

164 Hapa ameketi mwanamke mwingine, aliyeketi kule nyuma kabisa, nyuma kabisa, akinitazama moja kwa moja. Yeye, pia, ana mzunguko hafifu wa damu, pia. Alikuwa akiwaza hayo wakati huo huo. Sijapata kumwona mwanamke huyu maishani mwangu. Kwa kuwa huyo mwanamke mwingine alikuwa na kitu hicho hicho, nitazame. Je unaamini mimi ni nabii wa Mungu, ama mtumishi Wake? Una ugonjwa wa moyo. Iwapo hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa huna. Mungu, mwingi wa rehema Zake, naonyesha ya kwamba yu hai hapa katika jengo hili leo. Mungu mwingi wa rehema Zake! Amina.

165 Wanaweza kuwepo, wenye dhambi na waliorudi nyuma wangapi wanaoweza kusimama, na kusema, "Mungu, mwingi wa rehema Zake, unirehemu?" Simameni. Nitawaombeeni, mkiamini kwamba Yeye anataka . . . unahitaji rehema sasa. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki wewe na wewe. Uliyerudi nyuma, simama kwa miguu yako. Mungu mwingi wa rehema Zake! Una—una . . .

166 Kwa kweli hujafa ganzi mno, katika hali hii, hata ushindwe kuona kwamba hiyo ni ahadi ya majira haya. Kwa kweli hujafungwa mno katika dhehebu, na mambo mengine, hata

ushindwe kuona hii ni ahadi ya majira haya. Mungu mwingi wa rehema.

167 Yeyote yule, uliyesimama, ninakwenda kuomba kidogo. Nataka uingie katika kanisa linaloamini Injili yote na uka—na uka—na ukabatizwe ubatizo wa Kikristo, Mungu atakupa Roho Mtakatifu.

168 Je kuna mwingine ambaye atasimama, na kusema, "Mimi, nataka kukumbukwa. Mungu, katika rehema Zako, unikumbuke mimi. Sijaishi jinsi ilivyonipasa kuishi. Labda . . ."? Mungu akubariki, bibi. Na Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Vema. "Mungu, mwingi wa rehema Zake, unirehemu." Mungu akubariki, dada. Yupo . . .

169 Je kuna wangapi zaidi hapa, wasemao, "Nitasimama. Nataka Mungu ajue kwamba ninahitaji rehema. Sijaishi maisha mema. Nimeishi *hivi* na *vile*. Nimekuwa nikianguka na kusimama, ila sasa nahitaji rehema Zake." Mungu akubariki, ndugu. Mwingine, aseme, "Mungu mwingi wa rehema Zake!" Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni vema. Mungu mwingi wa rehema Zake! Mungu akubariki nawe, pia. Mungu akubariki kule nyuma. Mungu anakuona. Hebu simameni tu.

170 Mtasema, "Inafaa kitu, ndugu Branham?" Kabisa. Simama uone jinsi ilivyo tofauti.

171 Kama wewe u mwaminifu kabisa moyoni mwako, Mungu ni mwingi wa rehema. "Yeye hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba." Mungu mwingi wa rehema Zake! Ee Mungu, uturehemu.

172 Sasa wangapi hapa sasa, wenye hizi kadi za maombi? Ni zipi? Ni za A na za B, sivyo? Za A na za B. Wale wote wenye kadi za maombi za A, wajipange upande huu, na kadi za maombi za B wajipange nyuma yao.

173 Sijui kama kuna mtumishi yeyote hapa anayetazamia kunisaidia. Kama wapo, ningetaka wapande kuja huku, ningefurahia kupata msaada wenu—wenu hapa, kwani tutafurahia kuomba, na kuomba—kuomba pamoja nanyi.

174 Hii, Biblia inasema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ndiyo, bwana. "Kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya." Tumetenda hayo? Kwa neema ya Mungu; sio sisi, bali Mungu mwingi wa rehema akilitimiza Neno Lake. Mungu!

175 Basi, magari ya kusukumia wagonjwa, mkitaka kuyaweka mumu humu chini mbele; tutawaombea papa hapa, haitatulazimu kuyasukumia kule, sehemu yote ya nafasi ya katikati ya kanisa. Hebu waje moja kwa moja hadi hapa. Tutaomba kwa ajili ya kila mmoja, bila shaka. Mungu mwingi wa rehema Zake.

176 Tafadhali simameni kuelekea mkono wa kulia sasa, kwa dakika chache? Je Ndugu Brown alikuja pamoja nanyi? [Ndugu mmoja anasema, "Anakuja kesho."—Mh.] Anakuja kesho. Na—ni—nilitarajia kuwa angekuwa hapa. Wapi, Ndugu Outlaw yuko wapi, Ndugu Fuller yuko wapi? Baadhi ya wale watu waliokuwa pamoja nami nilipofika hapa kwa mara ya kwanza, turudi hapa. Mnakumbuka ile mistari ya maombi ya mitindo ya kizamani, tulipokuwa tunasimama pale hadi wakati mwingine iliwapasa mmoja anishikilie upande huu, na mmoja upande mwingine, kwani nilikuwa naishiwa nguvu mno?

177 Wangapi wamekwishakuwa kwenye mikutano hiyo siku hizo za nyuma huko mwanzoni? Tazameni hapa. Mnakumbuka siku za nyuma niliwaambia kuwa Bwana Yesu aliniambia kuwa kama ningekuwa mwaminifu, kuwa mambo haya yangelitokea. Ni sawa? Hatukuwa na mambo haya siku zile. Lakini ilitokea, kwa sababu Mungu ni mwingi wa rehema Zake, na ni mwaminifu kwa ahadi Yake. Amina! . . .? . . . Amina! Mungu asifiwe! Haleluya! "Lo, nina furaha mno kuwa mimi ni mmoja wao!" Amina. Jamani!

> Kuna watu karibu kila mahali,
> Ambao mioyo yao wote inawaka moto
> Kwa moto ulioshuka Pentekoste,
> Uliowasafisha na kuwafanya wasafi;
> Naam, unawaka moyoni mwangu sasa,
> Jina Lake litukuzwe!
> Nafurahi sana kwamba naweza kusema mimi
> ni mmoja wao.

178 Jamani, mimi, mtu mnyonge, mwenye mashaka, maskini fukara maskini na kipofu, jinsi nilivyokuwa; na sasa kwa rehema Zake, rehema Zake nyingi, naweza kuuona Ufalme wa Mungu ukiwa karibu. Amina. Amri Zake ni nzuri jinsi gani!

179 Simama hapo, ndugu yangu, kwa mikongojo yako. Kama huwezi kusimama, vyema, simama tu pale, tutashuka kuja kukuombea.

180 Na sasa basi hebu zile kadi A na B za maombi, wajipange msitari upande ule mwingine pale, tutawaombea.

181 Ndugu watumishi, bila shaka, kama mnaamini katika kuweka mikono juu ya wagonjwa, njooni moja kwa moja hapa msimame na mimi hapa madhabahuni. Tunakwenda kuwaombea wagonjwa.

182 Sasa kwenu ninyi mliosimama kwenye msitari ule, iwapo mwaweza kuamini kwamba Uwepo wa Mungu upo hapa, kwamba Roho Mtakatifu yupo miongoni mwetu sasa, akifanya yale hasa aliyosema angetenda. Kama ningekuwa na uwezo wa kuwaponyeni, bila shaka ningefanya hivyo. Kama ningelikuwa na njia yoyote ya kuwaponya, bila shaka ningefanya hivyo. Sasa sina. Ni . . . Mungu amenikirimu karama ndogo.

183 Mimi si mhubiri bora. Sina elimu ya kutosha kustahili kuwa mhubiri, katika hali ya uhubiri wa kisasa, ambapo—ambapo ujuzi unapaswa kuwa ujuzi wa kitheolojia, na lazima kuwa na shahada ya juu, na kadhalika. Mimi sijahitimu hayo. Lakini Mungu, akiona moyo wangu, na akijua kuwa ninataka kumfanyia jambo, napenda kufurahia hilo.

184 Mtu mmoja aliniambia hivi majuzi, akasema, "Nafikiri wewe ni mtu mwema tu, Ndugu Branham, bali nafikiri wewe katika uaminifu wako unakosea. Wewe uko nje kabisa ya nia. Je unajua utahukumiwa mwishoni?"

185 Nami nikasema, "Tazama nataka kukwambia jambo fulani. Nataka kusema kwamba wewe—wewe ungekuwa umesema kweli, kama kusudi lako ni kwa ajili ya ubishi tu. Kama mimi nimekosea, nami si—siamini kwamba nimekosea; lakini kama ningekuwa nimekosea, na nikafahamu sasa hivi kuwa ningeishi kufikia umri wa miaka mia moja, na mwishoni mwa maisha yangu angenihukumu, na aniambie, 'William Branham, Hustahili kuingia katika Mbingu Yangu. Toka uingie katika giza la nje.' Unajua nini? Ningemtumikia siku zote za maisha yangu mpaka niende, kwa vyovyote vile. Kwa maana nimepokea baraka Zake nyingi sana bila kustahili, hata Yeye ni zaidi ya uhai kwangu. Yeye ni kila kitu ambacho mimi . . . "

186 Yote mimi niliyo, yote ambayo ningalitumainia kuwa, nimepata kutoka kwa neema Yake na rehema. Nilikuwa mnyonge, na mwenye mashaka, maskini, kipofu; bali kwa neema Yake ameniponya, nami ni mwenye nguvu na afya, kwa neema ya Mungu. Nina macho mazuri. Nina vyakula, vinywaji, nina yote ninayohitaji. Hakuahidi kunitimizia matakwa yangu; mahitaji yangu.

187 Na kama nitatupiliwa mbali siku hiyo, nami nilijua . . . Siwezi kuona ambapo ningekuwa. Bali ningalijua kwamba nimekosea, na Mungu amenichagulia kukosea, ningalichagua kukosea, kwa maana nataka kutenda mapenzi Yake. Ni, kwa kuwa nampenda hata nataka mapenzi Yake yafanyike. Sasa, hilo ni tamshi kubwa, bali natumaini mnalipata katika roho ninayozungumzia ndani yake. Mnaona? Ninataka kufanya yaliyo mapenzi Yake. Ningemwomba neno fulani wakati mmoja, Naye akatikisa kichwa Chake na kusema "hapana," ningefurahia sana hilo kama tu wakati anaposema "ndiyo." Kwa maana, inatupasa kuomba daima, "Mapenzi Yako yatendeke." Hapana Zake ni bora tu kama . . . iwapo hayo ndiyo mapenzi Yake, hiyo ni bora tu kama . . . Ni bora zaidi kuliko ndiyo Zake, ikiwa ni mapenzi Yake kufanya hivyo. Hapo ndipo unapompenda sana. Amina.

188 Nianzapo kunena habari Zake, siwezi kukoma sasa. Jamani, Yeye ni halisi sana, halisi sana kwangu! Marafiki, Yeye—Yeye ni hali yote niliyo, yote ambayo kamwe ningaliweza kuwa, yote

ambayo ninatumaini kuwa, yana msingi wake katika Kristo Yesu, Neno Lake.

189 Ninashukuru usiku huu kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu, kwa Ujumbe huu. Najua yawezekana wengine kutokukubaliana Nao, bali kama nilivyowaambia, nina wajibu kwa Ujumbe fulani. Ishara ilitokea, na Mungu hatumi ishara kuonyesha tu ya kwamba Yeye ni Mungu. Ujumbe, Sauti fulani kila mara huandamana na ishara. Mtu yeyote ajua hayo.

190 Yesu alikuja pamoja na ishara na maajabu. Yeye alikuwa Mkuu sana alipokuwa akifanya ishara na maajabu, bali alipoanza kuketi na kuanza kuleta Ujumbe, "Mimi na Baba Yangu tu Mmoja," jamani, Lo, hiyo haikuwa hivyo kwao. Mwaona? Bali ile Sauti ilipaswa kufuata ishara ile.

191 Musa alipewa ishara mbili, na kila ishara ilikuwa na sauti. Naam. Nilihubiri hayo hapa siku zilizopita, mahali, fulani, kuhusu, *Sauti ya ile Ishara*. Haina budi kuwa na—na sauti ya ishara. Ni badiliko. Kila mara huwa hivyo. Kama haiko hivyo, basi haikutoka kwa Mungu.

192 Kama mtu yeyote akiinuka na huduma ng'eni na ya ajabu, ambayo inapatikana katika Biblia kuwa Kweli, na huyu mtu akae katika fundisho hilo la kale la kidhehebu, sahau hayo. Haina lolote! Mungu hatendi jambo kama hilo. Kitu hicho ni mana iliyooza, iliyo na mchwa, au mabuu, ama vyovyote unavyotaka kuviita, tangu miaka arobaini, hamsini iliyopita, akijaribu kula ile mana iliyoanguka miaka mingi sana iliyopita. Nao wana wa Israeli, safarini mwao, mana mpya ilishuka kila jioni. Naam, haikuhitajika kuhifadhiwa.

193 Sisi hatuishi kwenye wakati ambao tayari umekwishapita. Tunakula mana mpya, Mana ya sasa kutoka Mbinguni, tunapoendelea na safari.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

194 Bwana Mungu, Wewe ni halisi sana, Uwepo Wako. Nawaza juu ya neema, Bwana. Tu—tumekuona sasa hivi ukifanya mambo mengi sana! Tumekusikia Wewe ukinena kwa lugha, tukakuona ukitafsiri, kupitia kwa watu Wako. Ee Mungu, kukuona Wewe ukiponya wagonjwa, kufungua macho ya vipofu, kuwafanya viwete kutembea, viziwi kusikia, bubu kunena, Wewe ni Mungu Mkuu mwenye nguvu zote!

195 Na ndipo kuona ya kwamba uliahidi haya kwa ajili ya siku za mwisho. Ingawa tuna waigaji wa kimwili, bali haya yatangaza tu kwamba kuna Mungu halisi mahali fulani, aliye wa kweli kabisa. Nami naomba, Baba wa Mbinguni, usiku huu, kwamba tuwe na fahamu za kiungu sana hata tuone ya kwamba Wewe upo hapa.

196 Na hawa watu kwenye msitari, wanapopita kwenye msitari huu, Bwana . . . kwani tunafanya haya kwa sababu tuliwaahidi. Na Wewe ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na wale waaminio."

197 Hapa pana ndugu wahudumu wanaosimama hapa, watu ambao Wewe umewachagua kabla ulimwengu kuwekwa misingi, kwamba tungesimama hapa usiku huu. Ulijua kabla, hapajakuwako ulimwengu wowote, kwamba tungesimama hapa usiku huu, kwa sababu Wewe ni wa milele na milele.

198 Kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, usiku huu, kwamba hawa wagonjwa, viwete, vipofu, vilema, wenye kansa, chochote kile, wanapopita kwenye msitari huu, hebu wafahamu kwamba Mungu Yule Yule anayejua siri ya mioyo atawaponya iwapo wataikubali, watazame tu na kuelewa.

199 Mtu aliyemtazama yule nyoka wa shaba kama kipande tu cha shaba cha kuhani, asingaliponywa, kwa sababu hakufahamu ilikuwa nini.

200 Na leo, Bwana, ni hivyo hivyo. Kama wataiangalia karama, wakifikiria kwamba itaweza kuwasaidia, watakuwa hawana ufahamu. Ni uthibitisho wa Uwepo wa Mungu tu, uliopo hapa ili kuponya. Utupe hayo, Baba. Tunaomba haya yafanyike, katika Jina la Yesu. Amina.

201 Nataka kijana mmoja mpiga kinanda, mwanamume au mwanamke akipenda, yeyote yule, aende pale na kupiga wimbo huu, "Ni Tabibu wa karibu, Tabibu wa ajabu," akipenda, popote mpiga kinanda alipo. Basi huo . . .

202 Nakumbuka moja ya ibada zangu za uponyaji, Fort Wayne, Indiana. Msichana mdogo wa Ki-Amishi alikuwa ameketi, akipiga kinanda, "Ni Tabibu wa karibu, Tabibu wa ajabu. Mtoto mchanga aliletwa kwangu kwenye jukwaa, kiwete. Na nilipokuwa nikimwombea mtoto yule, aliruka kutoka mikononi mwangu na kukimbia pale jukwaani. Mama yake akazirai. Nyanya yake akatupa kitambaa chake, akaanza kulia.

203 Naye msichana huyu mdogo wa Ki-Amishi sasa, hajui chochote kuhusu Pentekoste, kwa kuwa ni mshiriki wa kanisa la Amishi; bali alikuwa akipiga kinanda. Nywele zake ndefu zikaanguka chini; akainuka kwa Roho na kuanza kunena katika lugha ng'eni, na kila . . . na kwa sauti ya wimbo ule. Na kile kinanda kikaendelea kujipiga chenyewe, kikiimba, "Ni Tabibu wa Karibu, Tabibu wa Ajabu." Amina! Ni Yeye Yule jana, leo na hata milele.

204 Basi na tuombe sasa . . . Basi hebu kila mmoja huko aombe. Ninyi pia watu mnapokuja msitarini, tunapowawekea mikono, kumbukeni, Yesu alisema, "Iwapo ungeamini, ungepona." Je, mnaamini hayo? Basi na tuimbe sasa.

> Ni Tabibu wa karibu,
> Tabibu wa ajabu,
> Na rehema . . . (Na tufungeni macho yetu tunapoimba)
> . . . za daima
> Ni dawa Yake njema.

Imbeni Malaika,
Sifa za Yesu Bwana;
Pweke limetukuka (Baba Mungu, wajalie watu
hawa sasa)
Jina Lake Yesu.

205 "Ni Tabibu . . ." Naam mnapopita sasa, Yeye yuko hapa. Aminini ninayowaambia, ama aminini wenyewe, Yeye yuko hapa. Kila mmoja kule na awaombee watu hawa.

206 [Ndugu Branham na wahudumu wawaombea wagonjwa huku Ndugu Borders akiongoza makutano kuimba. Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.]

Ee Bwana, naamini; Ee Bwana naamini;
Yote yatendeka, Ee Bwana, naamini.

207 Wote wanaoamini inueni mikono yenu *hivi*, mkaseme, "Naamini." [Makutano wanasema, "Naamini."—Mh.]

208 Huyu mtu aliyeketi hapa. Sababu yangu ya kunena naye sana, yeye anakufa kwa kansa. Yeye anatumia mkongojo huu. Huyu mtu hawezi kuishi kamwe, isipokuwa kwa ajili ya Mungu. Yeye ana kansa tumboni mwote, na atakufa isipokuwa kwa rehema Zake Mungu. Nami natumai ningali . . . [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] . . . neno la kumtia moyo mtu huyu.

209 Wewe, unajua madaktari hawawezi kukufanyia cho chote sasa. Umepita hayo, waona. Nawe una . . . Una nafasi moja tu, na hiyo ni katika Kristo, waona. Na, ndugu, wewe . . . Mimi nitafariki siku moja pia. Nawe pia huna budi kwenda, Yesu akikawia. Nami sina budi kukutana nawe kule, kusimama kule Hukumuni. Na usiku huu . . .

210 Wajua, kama ilivyo kwenye televisheni, televisheni huchukua hilo kila mara hata tunapojongeza vidole vyote, cho chote kile, kinarekodiwa. Kila neno tunalosema, limewekwa kwenye kumbukumbu. Naam, waona, televisheni imedhihirisha hayo. Naam, televisheni haitengenezi picha, huelekeza tu wimbi hilo kwenye televisheni. Mnaona, haitengenezi. Kulikuweko televisheni Adamu alipotembea duniani, kulikuweko televisheni Musa a—alipopitia kwenye Bahari ya Shamu, kulikuweko televisheni wakati Eliya alipokuwa mlimani Kameli, mwaona, bali waliivumbua tu hivi majuzi. Mwaona? Na sasa kila mahali mimi . . .

211 Kila tunapoenenda, kila sauti, inacheza sahani ya santuri tutakayoikuta kule hukumuni. Kila tendo tunalolitenda tutalikuta kule. Nitajibu kwa maneno ninayowaambia kama mhudumu. Mimi sina budi kufanya hivyo, kwa maana nitawajibika mbele Zake Mungu kwa hayo.

212 Basi kama ningaliweza, ningekuponya; kwa sababu umebakiza wakati mdogo, kama isingalikuwa kwa ajili ya Mungu. Naam, nimeshuka kuja kukukomboa, hayo tu ndiyo

nijuayo kutenda. Ndugu, cho chote ningalitenda kwa ajili ya mtu anayeketi pale katika hali hiyo, ningalitenda.

213 Na hebu ni kuulize, waona. Ta—ta—tayari umeponywa, kwa sababu Yesu alisema umeponywa. Mwaona, "Kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Kama waweza, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako, kukubali hayo, hautakufa, bali utaishi.

214 Sasa, waona, tunajua kuwa televisheni inapitia katika chumba hiki. Tunajua hayo. Hatuioni. Hatuwezi kuona, macho yetu hayajatengezwa vile, fahamu zetu haziwezi kuinasa. Inahitaji bomba lililotengenezwa, au chochote kile, kioo, kuinasa.

215 Vivyo hivyo Uwepo wa Mungu. Hatumuoni, bali tunajua Yeye yupo hapa. Yesu Kristo ni Yeye Yule. Tazama, Yeye tu hujitangaza Mwenyewe jinsi Yeye hujifanya Mwenyewe. Sasa, kuhusu uponyaji, kama angalikuwa amesimama hapa sasa hivi, asingelikutendea kitu zaidi, hata kimoja. Kama Mwana wa Mungu angesimama papa waona, hapa, na ndivyo Alivyosimama, Yeye yupo hapa. Wala hangefanya kitu zaidi kwako, kwa sababu tayari amekwishajitambulisha Mwenyewe hapa. Mwaona? Na Yeye yuko, papa hapa sasa, jinsi ile ile, kukuponya na kukufanya mzima.

216 Naye kijana mwanamke yule pale aliniambia, akisema, "Ulimwombea baraka, na kutabiri ama chochote kile juu yake, ya kwamba yeye angepata mtoto," akiketi kwenye kiti cha kusukumia wagonjwa. Naye akapata, akamzaa mtoto wake.

217 Na sasa kijana mwanamke aliyeketi hapa. Sasa alifanyiwa upasuaji wa tezi, na ikamfanya kupooza. Naam, tumeyaona mambo hayo yakitendeka sana. Basi dada mdogo, najua wewe u mkristo halisi. Kusudi la Mungu kukuruhusu kuketi pale, mimi sijui. Naamini labda ni kwa sababu ima . . . Imani, wewe—wewe unajaribu kupata imani, kutoka pale, waona; bali sasa tazama, tusijaribu tu kuwa nayo, na tuwe nayo sasa, waona, na ili tu—tuwe tunakwenda pale. Hivyo tu, itaanza sasa hivi, sasa tutakuwa wazima. Nanyi watu kwenye viti, popote pale mlipo, kumbukeni tu ya kwamba Kristo yupo hapa.

218 Sasa utasema, "Kuna mtu fulani, unaona picha yangu ikipita." Lo, ndivyo.

219 Hata maneno ya Yesu Kristo, aliyonena alipokuwa duniani, yanapitia tu katika jumba hili. Hayafi. Wangapi wanajua ya kwamba huo ni ukweli wa kisayansi? [Makutano wanasema, "Amina."—Mh.] Naam, sivyo? Ndipo Roho hutwaa hilo Neno lililoandikwa, na kulidhihirisha. Lo, utukufu!

220 Yupo hapa. Bwana yupo papa hapa sasa. Sisi tu . . . Tumeona mengi sana, Yeye ametenda mengi sana, hata sisi, mwajua, tunakwazika. Laiti tungalitambua si kitu fulani cha kubuniwa, jambo la kitheolojia; bali ushahidi kwamba Yeye aliahidi angejidhihirisha mwenyewe katika majira haya, yupo hapa

akiyaweka wazi haya mbele yetu sasa hivi. Ni ajabu jinsi gani! Si ajabu hiyo? [Makutano wanasema, “Amina.”—Mh.]

221 Basi aminini. Je, utaamini? Amini hutakufa. Utaishi na utampa Mungu utukufu. Utamtukuza Mungu. Je, umeshawahi kubatizwa? Wewe u Mkristo, sivyo? Na wewe u Mkristo. Vema, unataka kuishi kwa utukufu wa Mungu. Basi nenda ukaishi, ndugu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, uishi!

222 Na wewe dada, unataka kutembea kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kumtunza mtoto wako; Basi tembea, dada, katika Jina la Yesu Kristo!

223 Nanyi, kila mmoja wenu, fanya vivyo hivyo, katika Jina la Yesu Kristo! Msisahau hii Westward Ho Motel hapa usiku wa leo, Uwepo wa Mungu umetambulika hapa. Yeye hana upendeleo. Yeye anataka tu uamini. Je, mnamwamini Yeye sasa? [Makutano wanasema, “Amina.”—Mh.] Amina. Mungu akubariki.

224 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Sijui wamemchagua nani ku—kuruhusu watu waondoke. Ndugu Mushegian hapa, njoo papa hapa, ndugu. Atamalizia kwa maombi. Mungu awabariki. Mungu awabariki.

Mungu Aliye Mwingi Wa Rehema SWA65-0119
(The God Who Is Rich In Mercy)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne jioni, Januari 19, 1965, katika Ukumbi wa Hoteli ya Westward Ho, kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2014 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org